

JAMHURI YA MUUNGANO TANZANIA



OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM



Kumb. Na. DCC/CF.10/1

24/05/2023

TANGAZO LA NAFASI YA MWENYEKITI WA BODI YA SOKO LA SAMAKI FERİ – MAGOGONI LA HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM KWA KIPINDI CHA MWAKA 2023 HADI 2026

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam anawatangazia Wananchi kuwa kuna nafasi wazi ya Mwenyekiti wa Bodi ya Soko la Samaki Feri – Magogoni la Halmashauri ya jiji la Dar es Salaam kwa kipindi cha miaka mitatu 2023 hadi 2026.

SIFA ZA MWOMBAJI

1. Awe ni raia wa Tanzania na mkazi wa Dar es Salaam
2. Awe na umri usiopungua miaka ishirini na moja (21) na usiozidi miaka sitini na tano (65)
3. Awe na angalau Shahada ya Kwanza katika fani yoyote
4. Awe na uzoefu na amewahi kuonesha uwezo wake wa kuongoza katika shughuli za huduma za jamii
5. Awe na akili timamu
6. Asiwe amewahi kutiwa hatiani kwa kosa lolote la jinai
7. Asiwe na Wadhifa wa Kisiasa au uongozi wa ngazi yoyote katika Chama cha Siasa
8. Asiwe mtumishi wa Umma


TARATIBU ZA KUWASILISHA MAOMBI

1. Waombaji wote watume barua za maombi zikiwa na viambatisho vifuatavyo:
 - i) Nakala iliyothibitishwa ya cheti cha kuzaliwa au kitambulisho cha Taifa (Certified copy)
 - ii) Nakala zilizothibitishwa za vyeti vya masomo na Taaluma (Certified copies)
 - iii) Barua ya utambulisho kutoka kwa Mwenyekiti wa Serikali za Mitaa anapoishi ikiwa na picha ndogo ya hivi karibuni
 - iv) Wasifu binafsi (CV)
 - v) Barua kutoka kwa Wadhamini wawili (2) zikiwa na anuani kamili pamoja na barua pepe.

NB: Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 06 Juni, 2023

Barua zote za maombi zitumwe kwa anuani ifuatayo:-

*Mkurugenzi wa Jiji
1 Mtaa wa Mission
S.L.P. 20950
Halmashauri ya Jiji
11883 – DAR ES SALAAM*



Eng. Amani I.B. Mafuru

KAIMU MKURUGENZI WA JIJI

**KAIMU MKURUGENZI WA JIJI
HALMASHAURI YA JIJI LA DAR-ES-SALAAM**